

Salamu kutoka **ZIMBABWE!**


Zimbabwe iko Kusini mwa Afrika. Zaidi ya watu 16,500,000 wanaishi huko.

MAPOROMOKO YA MAJI YA AJABU

Maporomoko ya Maji ya Victoria huko Zimbabwe ni maporomoko makubwa ya maji ulimwenguni. Kishindo kinaweza kusikika umbali wa zaidi ya maili 24 (km 40)!



ZIARA KUTOKA KWA NABII



Mnamo Aprili 2018 Rais Nelson na Dada Nelson walifanya ziara Zimbabwe. Mamia ya watoto walimba "Mimi ni Mtoto wa Mungu" kwa ajili yao.

WANYAMA WA KUVUTIA

Kuna kanda nyingi za mbuga ndani ya Zimbabwe. Baadhi ya wanyama ambao wanaishi huko ni simba, viboko, twiga, swala na tembo.



SHUGHULI

Sanaa ya Tembo

Zimbabwe ina idadi ya pili kwa ukubwa ya tembo ulimwenguni!

1. Kata duara moja kubwa katika karatasi kwa ajili ya kichwa na duara mbili ndogo kwa ajili ya masikio. Kisha gundisha masikio kwenye kichwa.
2. Kata karatasi ndefu ya mstatili kutengeneza mkonga. Kunja mbele na nyuma ili utengeneze umbo la zig zag.
3. Kata pembe mbili za tembo.
4. Sasa chora macho na tabasamu kwa ajili ya tembo wako. Kisha gundisha pembe na mkonga juu yake!



LUGHA

Zimbabwe inazo lugha rasmi 16. Baadhi ya hizi ni Shona, Ndebele na Kiingereza—kwa kuzitaja chache tu!

MAELEZO YA UPISHI



Muriwo Unedovi (Siagi ya karanga ya Mboga)

Muriwo unedovi ni chakula cha asili huko Zimbabwe. Hapa kuna toleo unaloweza kujaribu!

1. Kata kata **kitunguu 1** na pika ndani ya sufuria yenyе **mafuta** kwa dakika 3–5. Kata kata **nyanya 2** na changanya kwenye sufuria. Pika kwa zaidi ya dakika 3–5.
2. Kata kata **vikombe 10 (ml 2400) za spinachi** (au mboga ya majani ya chaguo lako) na ongeza ndani ya sufuria. Acha mboga inyauke kwa dakika 5.
3. Ongeza **vijiko 2 vya kulia (ml 30) siagi ya karanga, robo ya kikombe (ml 59) maji, na 1/2 kijiko cha chai (ml 2.4) ya unga wa kitunguu saumu** Changanya vizuri na ongeza **chumvi** kwa ladha.

Hakikisha unapata msaada wa mtu mzima!